KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 13, Issue 2

12th Ramadhân 1432

12th Aug, 2011

YALIYOMO

KISIMAMO CHA USIKU 1 - 4

KISIMAMO CHA USIKU KATIKA MWEZI WA RAMADHAAN

Na: Sheikh Muhammad Naasir ud-Deen al-Albaani (رحمه الله)

Idadi ya raka'a za Qiyaam ni Kumi na Moja (11). Hii imetokamana na Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Haruhusiwi mtu kuongeza zaidi ya idadi hii, kwani Yeye (صلى الله عليه وسلم) hakuiongezea chochote kwenye maisha yake yote. Ingawaje, mtu anaweza kupunguza idadi ya raka'a hizi; anaweza mtu hata kuswali raka'a moja peke yake ya witr. Hii inaungwa mkono na vitendo vya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na maneno yake.

KUISWALI TARAWEEH KWA JAMAA'A

Imependekezwa kuswali Qiyaam katika mwezi wa Ramadhaan kwa Jamaa'a; na ni bora kuliko mtu kuiswali peke yake. Mtume (صلى الله عليه وسلم), yeye mwenyewe aliithibitisha: akaipendekeza: akaiafiki kutoka kwa Maswahaba zake (رضي الله عنهم), akaitekeleza yeye mwenyewe, na akaisisitiza kuhusu fadhla zake.

IDADI YA RAKA'A ALIZOSWALI MTUME (صلى الله عليه وسلم)

Riwaya Ya 'Aaisha (رضي الله عنها):

Abu Salamah Bin Abdur-Rahmaan alisimulia yakwamba alimuuliza 'Aaisha (رضي الله عنها) kuhusu alivyokuwa akiswali Mtume (صلى الله عليه وسلم). Nae ['Aaisha (رضي الله عنها)] akamjibu: "Iwapo ni katika mwezi wa Ramadhaan au mwezi mwengine wowote, Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kuswali zaidi ya raka'a kumi na moja. Alikuwa akiswali raka'a Nne [maana yake akitoa salamu moja] - na usiulize kuhusu uzuri au urefu wake. Kisha akaswali tena Nne - na usiulize kuhusu uzuri au urefu wake. Kisha akaswali Raka'a Tatu." (Imepokewa na al-Bukhaari, Muslim, Abu Uwaanah, Abu Daawud, at-Tirmidhee, an-Nasaa'ee, Maalik, al-Baihaqee na Ahmad).

Imaam an-Nawawee akaeleza katika sherehe ya Swaheeh Muslim, "Hii inaashiriya ruhusa ya kufanya hivyo (kuswali raka'a Nne na kutoa salaam moja). Ingawaje ni bora kutoa salaam baada ya kila raka'a mbili, kama ilivyokuwa kawaida ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), na inayokubaliana na amri ya kuswali swala ya usiku kwa jozi (mbili-mbili).

TANGAZO LA SWALA YA 'EID

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

TUNAFURAHA KUWATANGAZIA SWALAATUL 'EID ITAKAYOSWALIWA KATIKA UWANJA WA CONGO BOYS [MBARAKI POLICE] MWEZI UTAKAPO-ONEKANWA KATIKA ULIMWENGU WA KI-ISLAMU. SWALA ITASWALIWA SAA MOJA NA NUSU 7:30 AM ASUBUHI. TWAWAOMBA MUJE NA MISWALA YENU NA WUDHU WENU IN-GAWA MAJI NA MIKEKA ITAKU-WEPO . NAFASI ZA WANAWAKE PIA ZITAKUWEPO, NAO WAJITOKEZE KWA WINGI KAMA ILIVYO SUNNAH YA BWANA MTUME MUHAMMAD (صلى الله عليه وسلم)

Msimamo katika madh-hab ya Shaafi'ee, kama ilivyoashiriwa katika *al-Fiqhu 'alal Madhaahib il-Arba'ah*, sherehe ya al-Qastalaani ya al-Bukhaari na wengineo ni kwamba, "Inamlazimu mtu atoe *tasleem* baada ya kila jozi ya raka'a; na iwapo mtu ataswali Nne kwa *tasleem* moja, swala yake haitokubaliwa." Msimamo huu unapingana na hadeeth hii iliyo swaheeh, pamoja na ufahamu wa kisawasawa uliotangulia wa an-Nawawee, ambaye ni mmojawapo wa wanavyuoni wakubwa wa madh-hab hiyo. Kwahiyo, hakuna yoyote anayeruhusiwa kutoa fatwaa iliyo kinyume cha haya.

Katika riwaya nyengine, amesema Aaisha (رضي الله عنها): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali wakati wa usiku, katika mwezi wa Ramadhaan na miezi mengine, raka'a Kumi na Tatu, ambamo ndani yake palikuwa na raka'a Mbili za Fajr." [Imepokewa na Ibn Abee Shaybah, Muslim na wengineo].

Na vilevile katika riwaya nyengine, Aaisha (رضي الله عنها) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliswali raka'a Kumi na Tatu wakati wa usiku. Kisha baada ya kusikiya muadhini wa al-Fajiri, alikuwa akiswali raka'a mbili fupi." [Imepokewa na Maalik na kutoka kwake, al-Bukhaari na wengineo].

Kuhusu ikhtilafu iliyodhihiri baina ya riwaya mbili za mwisho, al-Haafidh Ibn Hajar akasema: "Pana uwezekano yakwamba, katika riwaya hii, 'Aaisha alijumlisha katika swala ya usiku pamoja na raka'a mbili za baada ya 'ishaa' ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizoziswali nyumbani, au raka'a mbili fupi ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizozianzilishia Qiyaam. Imethubutu katika swaheeh Muslim yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akianza swala zake za usiku kwa raka'a mbili fupi. Mimi naonelea hili

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

lililotangulia baadae kuwa na uwezekano wa usawa, kwa sababu riwaya ya Abu Salamah, ambayo yenye kuiwekea mipaka idadi kuwa Kumi na Moja, inaeleza hayo, 'Aliswali Nne kisha Nne kisha Tatu.' Haikutaja marejeo yoyote kuhusu raka'a mbili fupi zilizotajwa katika riwaya ya Maalik. Hili laruhusiwa, kwa sababu nyongeza kwenye riwaya inayofanywa na mpokezi aliye muangalifu (haafidh) inakubalika. Jambo hili limezidi kuthubutu kutokana na riwaya iliyopokewa na Ahmad na Abu Daawud kutoka kwa 'Abdullaah Bin Abi Qays kutoka kwa 'Aaisha aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali witr kwa raka'a Nne na Tatu, ..., au Kumi na Tatu. Hakuwa akiswali witr kwa zaidi ya Kumi na Tatu au kupungua chini ya saba." [Imepokewa na Abu Daawud, Ahmad, na wengineo kwa silsila nzuri ya wapokezi. Imeswahihishwa na al-Haafidh al-Iraaqi katika *Takhreej ul-Ihyaa'*].

Hii ndiyo riwaya iliyo swaheeh mno niliyoipata kwenye mas'ala haya, na kwa (riwaya) hiyo, mtu anaweza kuitatua ikhtilafu iliyodhihiri baina ya riwaya kutoka kwa 'Aaisha."

Ufafanuzi huu wa al-Haafidh vilevile umethibitishwa na riwaya ya Maalik kutoka kwa Zayd Bin Khaalid al-Juhanee aliyesimulia: "Katika usiku mmoja niliamua kumfuatilia kwa makini Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyokuwa akitekeleza swala yake ya usiku.

- Kwahiyo akaswali raka'a mbili fupi.
- Kisha akaswali raka'a mbili ndefu sana.
- Kisha akaswali raka'a mbili fupi kuliko mbili zilizotangulia.
- Kisha akaswali raka'a mbili fupi kuliko mbili zilizotangulia.
- Kisha akaswali raka'a mbili fupi kuliko mbili zilizotangulia.
- Kisha akaswali raka'a mbili fupi kuliko mbili zilizotangulia.
- Kisha akaswali witr (raka'a moja).

Hizo zikawa ni raka'a Kumi na Tatu." [Imepokewa na Maalik, Muslim, Abu Uwaanah, Abu Daawud, na Ibn Nasr]. Linalojitokeza hapa ni kwamba hizi raka'a mbili fupi ni Sunnah za Ishaa', kwa sababu hakuna riwaya zenye kuzitaja pamoja na raka'a Kumi na Tatu.

RIWAYA YA JAABIR

Amesimulia Jaabir Bin Abdillaah (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alituongoza sisi (usiku mmoja) katika mwezi wa Ramadhaan, kwa kutuswalisha raka'a Nane na witr. Katika usiku uliofuata, tulikusanyika msikitini, tukitarajia yakwamba atakuja tena (kutuongoza kwenye swala). Tulibakia hapo (tukimungoja) mpaka asubuhi. Kisha tukaingia (mpaka katikati ya msikiti) tukaanza kusema, 'Ewe Mjumbe wa Allaah! Usiku wa jana tulikusanyika msikitini tukitarajia yakwamba utatuongoza kwenye swala.' Ndipo nae alipojibu kwa kuwaambia: "Kwa hakika mimi nilikhofia yakwamba mutafaradhishiwa." [Imepokewa na Ibn Nasr, na at-Twabaraani katika *al-Mu'jam us-Swagheer*. Isnaad yake ni hasan kwa sababu ya hadeeth iliyotangulia. Katika *Fat-hul Baaree* na *at-Talkhees*, al-Haafidh aliashiriya uswaheeh wake, na akayafanya marejeo yake kwa Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan katika swaheeh zao].

RIWAYA YA IBN 'ABBAAS ILIYO DHA'EEF

Katika kuizungumzia hadeeth iliyotangulia ya 'Aaisha, al-Haafidh Ibn Hajar amesema: "Ama kuhusu yaliyopokewa na Ibn Abee Shaybah, kutoka katika hadeeth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali katika mwezi wa Ramadhaan raka'a ishirini na witr', ina isnaad iliyo dha'eef; zaidi ya hayo inakhalifiana na hadeeth ya 'Aaisha iliyopokewa kwenye swaheeh mbili. Na ('Aaisha) ni mjuzi zaidi kuliko watu wengine kuhusiana na hali na shughuli za Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika wakati wa usiku." [*Fat hul-Baaree* 4:205].

Kabla ya Ibn Hajar, al-Haafidh az-Zayla'ee nae akaeleza ufahamu kama huo. [Nasb ur-Raayah 2:153]. Kwa ujumla, hadeeth hii ya Ibn 'Abbaas ni dhaifu sana, kama iliyosemwa na as-Suyutee [*al-Haawee lil-Fataawee* 2:73]. Tatizo lake limechipuka kutoka kwa Abu Shaybah Ibraahim Bin 'Uthmaan, ambaye riwaya zake zimekataliwa, kama yalivyosemwa na al-Haafidh Ibn Hajar katika *at-Taqreeb.* Riwaya zote za hadeeth hii zina mpokezi huyu katika isnaad zake. [Imepokewa na Ibn Abee Shaybah katika *al-Musannaf*, 'Abd Bin Hameed katika *al-Muntakhab min al-Musnad*, at-Twabaraani katika *al-Mu'jam ul-Kabeer* na *al-Awsat*, pamoja na ukusanyaji kutoka katika *al-Mu'jam ul-Awsat* na adh-Dhahabi, na toleo la muungano wa *al-Kabeer* na *al-Awsat* na wegineo. Vilevile imepokewa na Ibn Adiyy katika *al-Kaamil*, al-Khateeb katika *al-Moowdih*, na al-Baihaqee katika *as-Sunan*. Riwaya zote hizi ndani ya isnaad zake kuna huyu mtu aitwae Ibraahim, kutoka kwa al-Hakam, kutoka kwa Muqsim, kutoka kwa Ibn 'Abbaas. Amesema at-Twabaraani, "Hadeeth hii haikupokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas isipokuwa kwa isnaad hii." Na al-Baihaqee akasema, "Hii imepokewa kutoka kwa Abu Shaybah; nae ni mtu dha'eef (katika kupokea kwake)." Vilevile al-Haythamee akasema (katika al-Mu'jam 3:172) yakwamba ni mtu dha'eef].

Kwa hakika huyu Abu Shaybah ni dha'eef mno, kama alivyoashiriya Ibn Hajar. Pia Ibn Ma'een akasema, "Si muaminifu." Al-Jawzajaanee akasema, "Aliuzulishwa (aliondolewa madarakani)." Shu'bah alimzingatia kuwa ni mrongo kwenye kisa alichosimulia. Na al-Bukhaari akasema, "Wao (wanavyuoni wa hadeeth) hawazitangazi riwaya zake." Kulingana na al-Haafidh Ibn Katheer: "al-Bukhaari akisema kumuhusu mtu yakwamba walikataa kutangaza riwaya zake (*sakatu 'anh*), maana yake ni kwamba amemuorodhesha kwenye daraja mbaya ya chini kabisa." [*Ikhtisaaru 'Ulum il-Hadeeth*].

Kwa ajili hii hadeeth hii na izingatiwe kuwa ni ya kuzua, hususan kwa vile imekhalifiana na hadeeth swaheeh zilizotangulia za 'Aaisha na Jaabir. Al-Haafidh adh-Dhahabi ameijumuisha hadeeth hii pamoja na za munkar (zilizokataliwa), na Ibn Hajar al-Haithamee akasema: "Ni dha'eef sana. Ma-Imaam (wanavyuoni wa hadeeth) walikuwa ni wakali katika kuwashutumu na kuwakosoa mmojawapo wa wapokezi wao. Alikuwa akipokea hadeeth ya kuzua, kama vile 'Hakuna Taifa lililoangamizwa isipokuwa katika mwezi wa March,' na 'Kiyama hakitosimama isipokuwa katika mwezi wa March,' Hadeeth hii kuhusiana na taraweeh ni miongoni mwa *munkar* zake. As-Subki ametangaza yakwamba, sharuti la kuikubali hadeeth iliyo dha'eef ni kwamba udhaifu wake na usiwe ni wa kupita kiyasi. Na adh-Dhahabi akasema: 'Yoyote ambaye Shu'bah atamzingatia kuwa ni mrongo, hadeeth yake na isizingatiwe kabisa.'" [al-Fataawee al-Kubra 1:195].

Tanabahi hapa yakwamba, al-Haithamee, katika kuthibitisha hoja kutoka kwa as-Subki imehusu ishara kwa mukhtasar yakwamba rai yake (al

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

-Haithamee) ni kwamba mtu hawezi kuswali raka'a ishirini. Baada ya kudondoa hadeeth ya Jaabir Bin Abdillaah, iliyopokewa na Ibn Hibbaan, as-Suyuti amesema: "Sisi tumefikia mapatano yakwamba kuswali raka'a ishirini haikuthibitishwa kwa kitendo chake (صلى الله عليه وسلم). Hadeeth iliyopokewa na Ibn Hibbaan inaunga mkono kikamilifu msimamo wetu wa kushikamana na aliyoyapokea al-Bukhaari kutoka katika hadeeth ya 'Aaisha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuswali, ema katika mwezi wa Ramadhaan au mwezi wowote mwengine, zaidi ya raka'a Kumi na Moja. Nayo (hadeeth ya Ibn Hibbaan) imeafikiyana nayo yakwamba aliswali taraweeh raka'a Nane zikifuatiwa na raka'a Tatu za witr, zikitimia jumla ya raka'a Kumi na Moja.

Yenye kuunga mkono haya, vilevile, ni kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa ni mwenye kuthibiti katika vitendo vyake, kama alivyoshikilia kuswali raka'a mbili baada ya 'Asr, licha ya uhakika yakwamba ni wakati ambao swala imekatazwa. Lau kama angeliwahi kuswali raka'a ishirini, basi hangeliwacha kufanya kitendo hicho. Na kama lingelifanyika hilo, basi halingelifichika kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) aliyesema yaliyotangulia." [*al-Haawee lil-Fataawee*].

Hii ni ishara ya nguvu yakwamba Imaam as-Suyuti amekubali kuswali raka'a Kumi na Moja, na kukataa kuswali ishirini kama ilivyo kwenye hadeeth iliyo dha'eef sana ya Ibn 'Abbaas.

RIWAYA KUTOKA KWA 'UMAR

'UMAR AAMRISHA WATU KUSWALI RAKA'A KUMI NA MOJA

'Umar (رضي الله عنه) aliwaamrisha watu waswali raka'a Kumi na Moja. Amesema as-Saa'ib Bin Yazeed (رضي الله عنه): "'Umar Bin al-Khattaab alimuamrisha Ubayy Bin Ka'b na Tameem ad-Daaree kuwaswalisha watu katika Qiyaam kwa raka'a Kumi na Moja. Msomaji alikuwa akisoma ayaat Mia Moja (katika kila raka'a), mpaka ikatubidi kuzielemea fimbo kwa sababu ya kisimamo kirefu. Hatukuwa tukimaliza isipokuwa kwa kuwasili alfajiri." [Imepokewa na Maalik katika al-*Muwattaa'* kutoka kwa Muhammad Bin Yusuf kutoka kwa as-Saa'ib Bin Yazeed. Isnaad hii ni swaheeh mno kwa sababu Muhammad Bin Yusuf alizingatiwa kuwa muaminifu na wanavyuoni; na Masheikh wawili (al-Bukhaari na Muslim) wamezikubali riwaya zake. As-Saa'ib Bin Yazeed ni Swahaba aliyefanya Hajj katika ujana wake pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم)]. Hii vilevile imepokewa na:

- Ibn Abee Shaybah (katika al-Musannaf) kutoka kwa Yahyaa Bin Sa'eed al-Qattaan.
- An-Naysaaburee kutoka kwa isma'eel Bin Umayyah, Usaamah Bin Zayd na Muhammad Bin Is-haaq.
- Ibn Khuzaymah kutoka kwa Ismaa'eel Bin Ja'far al-Madanee.

Na wote hao waliipokea kutoka kwa Muhammad Bin Yusuf kama ilivyokuja hapo awali.

Yafaa kuzingatiwa yakwamba katika riwaya yake, idadi aliyokuwa nayo Ibn Is-haaq ni "Raka'a Kumi na Tatu". Ibn Nasr ameipokea hivyohivyo katika *Qiyaam ul-Layl,* na akaongezea: "Ibn Ishaaq amesema, 'Kuhusiana na haya sijasikiya chochote kinachofaa na kukubalika kwangu kuliko riwaya ya as-Saa'ib; na sababu ni kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali raka'a Kumi na Tatu usiku.'"

Idadi hii (Kumi na Tatu) ilikuwa ilitajwa na Ibn Is-Haaq peke yake. Imeafikiyana na mojawapo ya riwaya zilizotangulia kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) kuhusu swala ya Mtume ya usiku, ambapo aliashiriya yakwamba raka'a mbili ya hizo raka'aat zilikuwa ni Sunnah za al-Fajr. Riwaya ya Ibn Is-Haaq inaweza kufasiriwa hivyohivyo, ikawa inakubaliana na wapokezi wengine.

Kutokamana na yaliyotangulia, tumetambua makosa ya wazi katika matamshi ya Ibn Abdul Barr, "Mimi simjui yoyote aliyepokea raka'a Kumi na Moja isipokuwa Maalik." Al-Mubaarakfuri akazungumza kuhusu matamshi haya, "Huku ni kuelewa vibaya kusikofaa." [Tuhfat ul-Ahwaathee].

Vilevile az-Zarqaanee aliyakosoa matamshi ya Ibn Abdul-Barr kwa kusema: "Matamshi haya si sawa! Riwaya (kuhusiana na 'Umar) ime [pokewa kwa isnaad tafauti, kutoka kwa Sa'eed Bin Mansoor, kutoka kwa Muhammad Bin Yusuf, aliyesema, 'Raka'a Kumi na Moja,' sawa na aliyoyahifadhi Maalik." [Sherhe ya al-Muwattaa'. Isnaad ya riwaya hii ni swaheeh isiyo na shaka yoyote, kama ilivyoelezwa na as-Suyuti katika al-Masaabih. Hii peke yake inatosha kuikataa kauli ya Ibn Abdul-Barr; Jee iwapo tutaongezea juu yake riwaya nyengine zenye kuunga mkono zilizotangulia kutajwa hapo awali]?

IDADI YA RAKA'A YA TARAWEEH YENYE KURUHUSIWA

Tumeshathibitisha yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Maswahaba zake (رضي الله عنهم) waliswali raka'a Kumi na Moja katika Qiyaam. Hii ndiyo idadi swaheeh ambayo waliyopokewa kuiswali, pasi na kuzidisha kitu, katika Ramadhani na nyakati nyengine katika mwaka mzima.

Hakuna riwaya iliyo swaheeh yenye kuthibitisha yakwamba palikuwa na Swahaba yoyote aliyeswali raka'a ishirini za *taraweeh*. Bali, imethubutu yakwamba 'Umar (رضي الله عنه) aliwaamrisha watu waswali raka'a Kumi na Moja, muafaka na kitendo swaheeh kilichopokewa cha Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwahivyo, ni waajib kushikamana na idadi hii, bila ya kuongezea kitu, kufuatia amri yake (صلى الله عليه وسلم): *"Wale miongoni mwenu watakaoishi baada yangu wataona ikhtilafu nyingi. Kwahiyo, shikamana na Sunnah zangu, na Sunnah za Makhalifa waongofu; shikamaneni nazi kisawasawa, ziumeni kwa meno (magego), na mujihadhari na mambo ya kuzua (katika Dini), kwa sababu kila jambo la kuzua ni bid'ah, na kila bid'ah ni kitendo cha upotofu."*

Kwenye haya maneno ya mwisho, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaongezea katika hadeeth nyengine: "Na kila kitendo cha upotofu, mwisho wake ni motoni."

Ni jambo maarufu sana yakwamba wanavyuoni wamekhitilafiana kwenye mas'ala mengi ya fiqh, miongoni mwayo ikiwemo haya mas'ala ya idadi ya raka'a ya taraweeh. Twaona kwenye suala hili rai sampuli nane zilizo tafauti: "Arubaini na Moja, Thalathini na Sita, Thalathini na Nne, Ishirini na Nane, Ishirini na Nne, Ishirini, Kumi na Sita na Kumi na Moja." [Al-'Ayni amepokea rai hizi (5: 356-357), na kisha akataja yakwamba idadi ya mwisho ndiyo ambayo iliyochaguliwa na Imaam Maalik, na vilevile Abu Bakr Bin al-'Arabee]. Hadeeth hiyo iliyotangulia hapo juu inaashiriya njia ya kutatua ikhtilafu yoyote inayotokea baina ya Waislamu. Kwa vile suala hili ni jambo ambalo watu walilokosana kwalo, tulitatue kwa kuregea kwenye Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambayo si chochote isipokuwa ni kuswali raka'a Kumi na Moja. Kwa hakika ni waajib kufuata hilo, na kutupilia mbali lolote lenye kwenda kinyume chake - hususan iwapo Sunnah

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

za Makhalifa waongofu (Khulafaa) inaafikiyana nayo vilevile.
Lau kama idadi ya nyongeza, juu ya riwaya swaheeh ya Kumi na Moja, ingelikuwa imethubutu kutoka kwa miongoni mwa Makhalifa waongofu na wengineo katika wanavyuoni wa Maswahaba, basi tungelishindwa ikatubidi tukubali kuruhusu kwao. Sababu ya haya ni kwamba sisi twaamini ilimu yao na fadhla zao, kukataa kwao mambo ya kuzua katika Dini, na kuhusika kwao kukubwa katika kuwakataza watu kuzua. Hatahivyo, kwa vile hapana chochote katika haya kilichothubutu kutoka kwao, kama ilivyothibitishwa hapo juu, sisi hatuzingatii nyongeza yoyote kuwa ni yenye kuruhusiwa. Hili, twataraji litaleta ukumbusho kwa wale wenye kudai yakwamba wanawapenda Maswahaba na kupendelea kulinda mafunzo yao. Mlinzi wa kweli wa Maswahaba ni yule mwenye kuzifanyia utafiti riwaya zitokazo kwao, na kisha ashikamane nazo.

BAADHI YA MANENO YA WANAVYUONI

Idadi ya wanavyuoni wakubwa wameshikilia msimamo yakwamba hairuhusiwi kuswali zaidi ya raka'a Kumi na Moja. Miongoni mwao ni Imaam Maalik (katika riwaya mojawapo itokayo kwake). Amesema As-Suyuti: "Al-Juri, [kuna idadi ya wanavyuoni wa ki-Shaafi'ee wenye Jina hili la ukoo. Haieleweki ni yupi miongoni mwao as-Suyuti aliyemkusudia hapa], mmojawapo wa Marafiki zetu, amepokea yakwamba Maalik alisema, "Idadi ya raka'a ambazo 'Umar Bin al-Khattaab alizowakusanya watu juu yake inapendekeza zaidi kwangu - ambayo ni raka'a Kumi na Moja. Vilevile ilikuwa ndiyo swala ya Mtume (صلى الله عليه وسلم).' Aliulizwa, Raka'a Kumi na Moja ikiwemo witr?' Akajibu, 'Na'am: na raka'a Kumi na Tatu ni karibu na hiyo (katika usawa) [Hapa alikuwa akikusudia baadhi ya riwaya swaheeh kutoka kwa 'Aaisha zilizotajwa hapo awali, zikiwemo ndani yake raka'a mbili za 'Ishaa']. Kisha akaongezea, 'Na mimi sifahamu ni kutoka wapi watu walizua hizi raka'a nyingi namna hii.'" [*al-Masaabeeh fee swalaat at-Taraaweeh* (*al-Fataawee* 2:77)].
Imaam Ibn ul-'Arabi amezitaja riwaya zenye kukhitilafiana kutoka kwa 'Umar, na rai yakwamba hakuna idadi maalum katika raka'a za taraweeh. Kisha akasema: "Msimamo wa sawa ni kuswali raka'a Kumi na Moja, ambao ndiyo njia ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyoswali Qiyaam.Idadi zote nyengine hazina dalili au msingi wowote. Lau kama tungeliweka kiwango, basi iwacheni iwe ni idadi aliyoiswali Mtume (صلى الله عليه وسلم). Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kuswali katika Ramadhaan au katika miezi mengine zaidi ya raka'a Kumi na Moja. Hii ndiyo swala ya Qiyaam; na mtu analazimika kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika kuiswali." [Sharh at-Tirmidhee (4:19)].
Imaam Muhammad Bin Ismaa'eel as-San'aani alithibitisha yakwamba idadi ya ishirini katika taraweeh ni bid'ah. Kisha akasema: "Na hakuna chenye kustahiki kusifiwa katika bid'ah. Bali, kila bid'ah ni kitendo cha upotofu." [Subul as-Salaam].

KUWADHARAU (KUWATWEZA) WANAVYUONI WAKUBWA

Tuanapotia mkazo katika kushikamana na idadi ya taraweeh iliyothubutu kwenye Sunnah, hii haimaanishi hata chembe kuwa sisi twawadharau wanavyuoni wenye kukubali idadi za ziyada, au kwamba twawanasibisha na mambo ya uzushi. Sisi hatuamini yakwamba wanavyuoni wakubwa wameegemeza rai zao juu ya matamanio ya nyoyo, lakini wameegemeza rai zao juu ya uwanachuoni wa kihakika na kupambana kwa kusubiri kufikiya kwenye Haki. Kwahiyo, wao watakuwa ni wenye kulipwa katika hali zote (Inshaa-Allaah) kama alivyosema 'Amr Bin al-'Aas yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Atakapohukumu hakimu kwa Ijtihaad, na akafikiya kwenye Ukweli, atapata malipo mara mbili. Na iwapo atahukumu kwa Ijtihaad, na akakosa kupata ukweli, atapata malipo mara moja."*
Sisi hatuwezi kuzikataa fadhla alizonazo mwanachuoni juu yetu; wao ndiwo waliotuongoza sisi kupitia kwenye njia ya ilimu, na wakatufundisha umuhimu wa Kitaab na Sunnah, na kwamba inatupasa kuvithamini vitu hivyo kuliko rai zozote zenye kwenda kinyume nazo. Kwa mfano Imaam ash-Shaafi'ee amesema: "Wameafikiyana Waislamu yakwamba itakapomdhihirikia mtu yoyote, Sunnah kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), basi haifai kwake kuiwacha Sunnah hiyo kwa ajili ya rai ya mtu yoyote." [ar-Risaalah].
Zaidi ya hayo ni kwamba kukhitilafiana na baadhi ya wanavyuoni kwenye mas'ala haya haimaanishi yakwamba sisi tunajizingatia kuwazidi wao kwa ilimu na ufahamu.Hayo si kweli, bali ni dhana zisizofaa. Sisi twajua kwa yakini yakwamba ma-Imaam wanne wana ilimu kuliko wanafunzi wao na wale waliokuja baada yao. Na juu ya hayo, wanafunzi wao walikhitilafiana nao kwenye mas'ala mengi. Na jambo hili ni lenye kuendelea kutokeza katika kila vizazi vinavyofuatana; wanavyuoni waliokuja baadae wakikhitilafiana na wanavyuoni wa zamani - maadamu kunaendelea kuwepo wanavyuoni wenye 'Ilmu miongoni mwa Waislamu. Wanafunzi hawa wanapokhitilafiana na waalimu wao, hapana anaefahamu yakwamba wao wanadai kuwa ni bora kuliko wao.
Kwa hakika, msimamo wetu na ma-Imaam hawa ni kama ilivyosema 'Aasim Bin Yusuf [nae alikuwa ni mwanafunzi wa wanavyuoni wawili wakubwa, Muhammad na Abu Yusuf], aliyeambiwa, "Kuna mas'ala mengi ambayo wewe umekhalifiana na Abu Haneefah." Nae akajibu, "Abu Haneefa amepewa (katika 'Ilmu na ufahamu) katika ambayo sisi hatukupewa. Ufahamu wake ulifikia kiwango ambacho sisi hatuwezi kufikia. Ama kutuhusu sisi, ufahamu wetu hauwezi kupita zaidi ya kiwango chetu. Na sisi hatuwezi kutoa fatwaa kulingana na maneno yake mpaka tuweze kufahamu msingi wake wa aliyoyasema." [Imepokewa na Fillaanee katika 'Iqaadh ul-Himaam (Uk. 51-52 kutoka kwa mwanachuoni Abu al-Layth as-Samarqandee)].
Hapa 'Aasim alikuwa akikusudia maneno mashuhuri ya Abu Haneefa, "Hairuhusiwi kwa yoyote kuchukuwa rai zetu mpaka ajue tumeitegemeza juu ya nini." Kwahiyo, ukweli wa mambo ni kwamba, yeye alikuwa akijiegemeza kwa Abu Haneefa, hata kama anakhitilafiana nae! Sisi tunasema hayo ya hapo juu haliyakuwa, wakati huo huo tunathibitisha yakwamba rehma za Allaah ni kunjufu kuliko kuifungamanisha 'Ilmu na fadhla zake kwa hawa ma-Imaam wanne peke yao. Kwa hakika, Allaah (سبحانه وتعالى) ana uwezo wa kuumba baada yao wenye 'ilmu kwenye baadhi ya mas'ala. Pia mtu wa hali ya chini anaweza kuwa na 'Ilmu asokuwa nayo mtu aliye na hali bora. Hili ni jambo maarufu miongoni mwa wanavyuoni, na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Taifa langu ni kama mvua; hapana uwezekano wa kueleza iwapo uzuri wake upo mwanzoni au mwishoni mwake." [Imepokewa na at-Tirmidhee (aliyeithibitisha kuwa hasan), al-'Uqailee, na wengineo, kwa isnaad mbalimbali].